

## **HOMA YA MAPAFU YA NG'OMBE (Contagious Bovine Pleuro-pneumonia, CBPP)**

### **Na Augustino Chengula**

Mlipuko wa ugonjwa wa Homa ya Mapafu ya Ng'ombe uliripotiwa kwa mara ya kwanza katika Tarafa ya Loliondo maeneo ya Sonjo mwaka 1921 na 1928 na ulisambaa katika maeneo mbalimbali ya nchi; Mwaka 1992 ugonjwa huu ulilipuka mkoani Kagera ukitokea kusini mwa Uganda. Mwaka 1995 ugonjwa huu ulionekana mkoani Morogoro na baadaye kuenea maeneo mbalimbali ya nchi. Serikali iliweka mikakati ya kudhibiti ugonjwa huu kupitia mpango wa

Roll back Vaccination. Idadi ya ng'ombe walioathirika na ugonjwa huu

inaendelea kupungua kutoka ng'ombe 3,523 hadi ng'ombe 22 mwaka 2010. Ugonjwa huu umedhibitiwa katika mikoa iliyoko kusini mwa reli ya kati, hususan katika mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Kati na Magharibi na uchanjaji unaendelea katika mikoa ya Kanda za Ziwa na Kaskazini.